KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

MASJALA YA MUSOMA

ILIYOPO MUSOMA

RUFAA YA ARDHI NA. 10 YA 2022

(Imetokana na Maombi ya Ardhi No. 147 ya 2021 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Mkoa wa Mara linaloketi Musoma)

SAMWEL IKANGALA MPELA .....MRUFANI

DHIDI

LOYCE MIRUMBE NYAMWASHA ..... MRUFANIWA

HUKUMU

05 Juni, 2023

M. L. KOMBA, J.:

Ndoa ni muunganiko wa hiyari baina ya mke na mume ambao wamekusudia kuishi pamoja. Hii ni kulingana na kifungu cha 9 cha Sheria ya Ndoa, Sura 29 ya Shera za nchi (Sheria ya ndoa).

Kifungu cha 160 cha Sheria hiyo hiyo ya Ndoa kimetoa uwezo kwa Mahakama kutamka dhana ya ndoa kwa mwanamke na mwanamume walioishi kwa miaka miwili au zaidi kama mume na mke na jamii kuwapa heshima ya mume na mke. Mahakama inapotamka dhana ya ndoa na baadaye ndoa hiyo kuvunjika, inaweza kuendelea kutoa maamuzi kuhusu

matunzo ya mke na watoto kama wapo na endapo mke ataomba matunzo; au kutoa uamuzi kuhusu suala lolote kwa kadri itakavyoona inafaa kwa mke na mume walioishi kwa dhana ya ndoa ikiwa ni pamoja na mgawanyo wa mali iliyochumwa kwa pamoja wakati wa dhana ya ndoa. Tazama kesi ya **Hemed S.Tamim vs. Renata Mashayo** [1994] TLR, 197.

Mkata rufaa katika kesi hii ndugu Samwel Ikangala Mpela anayefuatilia hatima ya nyumba iliyopatikana wakati anaishi kinyumba na mjibu rufaa hajaridhika na maamuzi ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Mkoa wa Mara lililoketi Musoma (Baraza) na kuamua shauri la Madai Na. 147 la Mwaka 2021 kwamba Baraza haliwezi kusikiliza shauri lenye msingi wa madai ya Talaka. Maamuzi haya yalitokana na mkata rufaa kuomba Baraza litamke kuwa nyumba iliyojengwa kwenye kiwanja Namba 596 Kitalu 'H' Mtaa wa Mburumatare katika mji wa Bunda ni mali ya mkata rufaa na mjibu rufaa iliyopatikana wakati wa dhana ya ndoa.

Baraza baada ya kusoma nyaraka za rufaa na hata bila kuwasikiliza wahusika iliamua;

> *'Madai yanavyoonekana ni madai ya kindoa, hivyo Baraza hili linayaondoa kwa kukosa mamlaka. Wadaawa wanaelekezwa wapeleke mgogoro kwenye Mahakama yenye mamlaka'.*

Maamuzi haya hayakumfurahisha mkata rufaa na hivyo kuwasilisha rufaa yake Mahakamani hapa akiwa na sababu mbili za rufaa kwamba;

1. *Mwenyekiti wa baraza alikosea kuyaondoa maombi yake kwa kusema Baraza halina uwezo kusikiliza maombi yale bila ya kuwapa nafasi wadaawa kujieleza.*
2. *Mwenyekiti wa Baraza alikosea kuyaondoa maombi yake bila kuzingatia kwamba maombi ya mkata rufaa yalitokana na rufaa ya madai na. 06 ya mwaka 2020 katika Mahakama ya Wilaya Bunda ambapo alielekezwa kufungua shauri katika Baraza hilo.*

Rufaa yake mkata rufaa ilipangwa kusikilizwa leo Mahakamani hapa na kila upande ulifika mahakama kwa wakati bila uwakilishi, walijieleza wenyewe.

Alipopata wasaa mkata rufaa kuieleza mahama hoja zake za rufaa alieleza kwamba aliishi na mjibu rufaa kama mke na mume tangu mwaka 1995, na kwamba mwaka 1997 alijipatia eneo na kuanza kujenga nyumba ambapo walihamia kwenye nyumba hiyo mwaka 2002 na kuendelea kuishi na mjibu rufaa kama mke wake.

Katika mwaka 2013 Serikali ilianzisha utaratibu wa kurasimisha maeneo na hivyo eneo walilojenga nyumba yao lilipimwa na kupatiwa namba ya kiwanja 596 kitalu 'H'. Alieleza zaidi kwamba alipompa pesa mjibu rufaa akalipie hati ya nyumba, mjibu rufaa aliandika jina lake peke yake kwenye hati ya kiwanja. Alipelekea malalamiko kwenye Ofisi za Ardhi kuomba mabadiliko ya majina lakini alishindwa kwa kuambiwa waende wakaelewane.

Alipoona hapati manufaa aliijulisha Makahama hii kuwa alifungua shauri la Talaka Na. 54 la mwaka 2019 katika Mahakama ya Mwanzo Bunda ambayo ilionesha kutambua dhana ya ndoa baina ya pande hizi mbili **lakini haikueleza lolote kuhusu mali iliyopatikana wakati wanaishi pamoja**. Alieleza zaidi kwamba mjibu rufaa hakukubaliana na maamuzi na aliamua kufunga milango ili mkata rufaa asiingie ndani, alifungua shauri la madai Mahakama ya mwanzo (Na. 238 la 2019) ambapo iliamriwa kuwa nyumba inayobishaniwa ni mali halali ya mjibu rufaa. Alipokata rufaa Mahakama ya wilaya (rufaa ya madai na. 6 ya mwaka 2020) maamuzi yaliyofanywa kwenye shauri na. 238 ya 2019 yalifutwa kwa maelezo kwamba Mahakama haikuwa na uwezo wa kusikiliza shauri lililohusu nyumba na mkata rufaa alishauriwa kufunga madai katika Baraza ambapo Baraza limeiondoa kesi hiyo.

Mkata rufaa hakuridhika na maamuzi ya Baraza kwa vile alielekezwa kufanya hivyo na Mahakama ya Wilaya na ameiomba mahakama hii kutoa amri ya kulipwa kiasi cha shilini 40,000,000/ ambayo ni thamani ya nyumba inayobishaniwa au nyumba iuzwe na fedha itakayopatikana igawanywe kwa pande zote mbili.

Mjibu rufaa aliieleza Mahakama hii kwamba katika baraza la Kata maamuzi yalikuwa upande wake na mkata rufaa akafungua madai katika Baraza la Ardhi na nyumba ambapo alilalamika kuhusu mali ya ndoa na alielekezwa kufungua shauri la talaka Mahakama ya Mwanzo. Alifanya hivyo kupitia shauri la Talaka na. 54 ya mwaka 2019 ambapo kwa maelezo ya mjibu rufaa, iliamriwa kuwa hapakuwa na ndoa. Mjibu rufaa alieleza zaidi kuwa baada ya maamuzi hayo mkata rufaa alianza kufungua kesi sehemu mbalimbali na sehemu zote mjibu rufaa alishinda. Alieleza katika Baraza kesi mbili zilifunguliwa na ya pili ilikuwa madai Na. 147 ya Mwaka 2021 ambapo iliamriwa kuwa ni suala la ndoa. Mjibu rufaa amelalamika kuwa mkata rufaa anamsumbua kufungua kesi nyingi wakati suala lao lilishapata suluhu katika Mahakama ya Mwanzo tangu mwaka 2019 (kupitia shauri la Talaka Na. 54 ya mwaka 2019) na aliiomba Mahakama hii kumaliza usumbufu anaoupata.

Baada ya kusoma nyaraka ya rufaa na kuwasikiliza wahusika nimegundua jukumu la Mahakama hii ni kuamua endapo Baraza lilikuwa na uhalali kuyaondoa maombi Na. 147 ya Mwaka 2021 kwamba yanahusu masuala ya ndoa.

Nimesoma hati ya madai iliyowasilishwa katika baraza tarehe 04/11/2021 katika ukurasa wa 3 nafuu aliyoomba mkata rufaa ilikuwa;

> *'Baraza hili tukufu litamke kuwa nyumba yenye mgogoro ilichumwa kwa nguvu ya pamoja kati ya mwombaji na mjibu maombi wakati wa dhana ya ndoa.'*

Kutokana na kiziduo hicho (excerpt) ni wazi kuwa msingi wa madai ni mali inayodhaniwa kuchumwa pamoja wakati wa dhana ya ndoa. Tuone sasa mamlaka ya Baraza la Ardhi na Nyumba kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 3 cha Sheria ya Migogoro ya Ardhi, Sura ya 29 ya Sheria;

> *'3.-(1) Subject to section 167 of the Land Act and section 62 of the Village Land Act, every dispute or complaint concerning land shall be instituted in the Court having jurisdiction to determine land disputes in a given area. (2) The Courts of jurisdiction under subsection (1) include- (a) the Village Land Council; (b) the Ward Tribunal; (c)* ***the District Land and Housing Tribunal****; (d) the High Court; or (e) the Court of Appeal of Tanzania.' Ikiwa na maana vyombo vyenye uwepo za kusikiliza migogoro ya ardhi ni Pamoja na Baraza.*

Kifungu cha 167 cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 kinaeleza;

> *'167-(1) The following courts are hereby vested with exclusive jurisdiction, subject to the provisions of this Part, to hear and determine all manner of disputes, actions and proceedings concerning land, that is to say-*

(a) the Court of Appeal;

(b) the High Court;

(c) The District Land and Housing Tribunal;

(d) Ward Tribunals;

(e) Village Land Council.'

Ikiwa na maana kwamba miongoni mwa mabaraza na mahakama yaliyotajwa hapo juu Baraza linao uwezo wa kusikiliza mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi.

Viziduo hivyo nilivyovirejea vinaeleza majukumu ya Baraza la Ardhi na Nyumba (Baraza) kwamba lilianzishwa kwa lengo la kutatua migogoro ya ardhi. Masuala ya ndoa na talaka yanasimamiwa na Sheria ya Ndoa na imetaja Mahakama ya Mwanzo kuwa na uwezo wa kisikiliza mashauri ya talaka kwa wanandoa.

'75. A primary court shall have jurisdiction to entertain a suit under this Part where the parties were married in accordance with customary law or in Islamic form or, in the case of a suit under section 69 or section 71, if the court is satisfied that had the parties proceeded to marry they would have married in accordance with customary law or in Islamic form.' Ikiwa na maana kwamba Mahakama ya Mwanzo ndio yenye uwezo wa kusuluhisha wanandoa.

Nikirudi kwenye hoja ya msingi wa rufaa hii ni kwamba mkata rufaa aliliomba Baraza kutamka kuwa nyumba yenye mgogoro ilichumwa kwa nguvu za

pamoja baina yake na mjibu rufaa. Mgogoro unaohusika hapa ni ule wa namna nyumba ilivyojengwa. Ikiwa ilijengwa kwa nguvu za pamoja suala hili linahuska na maisha ya ndoa na hivyo sio jukumu la Baraza kuamua kama nguvu za pamoja ndio zilisaidia kujengwa kwa nyumba husika. Hivyo naona Baraza lilikuwa sahihi kueleza kuwa madai yalihusika zaidi na masuala ya ndoa. Ni kama nilivyorejea kifungu cha Sheria na kama wadaawa wenyewe walivyoeleza kwamba Mahakama ya Mwanzo kupitia kesi ya Talaka ilitoa uamuzi kuhusu dhana ya ndoa, Mahakama hiyo ndio ilikuwa sahihi kutoa hatma ya mali iliyochumwa pamoja.

Hii ikiwa ni rufaa ya kwanza, Mahakama imepata wasaa wa kusoma nyaraka mbalimbali kuhusu kesi hii ikiwemo hukumu ya Shauri la Talaka Na. 54 la mwaka 2019 na kujiridhisha kwamba katika ukurasa wa 12 wa hukumu Mhe. Hakimu alieleza;

> '*...hivyo basi katika shauri hili hakuna shaka kuwa SM1 na SU1 (mkata rufaa na Mjibu rufaa) wamekuwa wakiishi kama mke na mume lakini si mke na mume... haki alozonazo SM1 ni kama zilivyoainishwa katika kif cha 160(2) ambazo ni matunzo kwa mwanamke, matunzo ya Watoto na mgawanyo wa mali, ndizo haki alizonazo mdai, kulingana na sheria hii.*'

Baada ya maamuzi hayo Mkata rufaa aliieleza mahakama hii alirudi kwenye nyumba ila alishindwa kuingia ndani, alifungiwa nje. Mahakama hii inaona Mahakama ya mwanzo haikumalizia jukumu lake la kugawanya mali iliyopatikana katika dhana ya ndoa kama alivyoeleza. Jambo hili sio sawa kwa vile hata Mahakama ya Rufaa ilishaeleza kuwa ikiwa wadaawa waliishi pamoja hata kama dhana ya ndoa inapingika Mahakama inapaswa kugawanya mali iliyopatikana. Soma maamuzi katika kesi ya **Hemed S.Tamim vs. Renata Mashayo.** (yalisharejewa).

Hadi kufikia hapa Mahakama hii inaona Baraza lilikuwa sahihi kuyaondoa maombi Na. 147 ya Mwaka 2021 na rufaa hii inatupiliwa mbali. Ikiwa Mkata rufaa anaona bado anayo madai kuhusu nyumba anashauriwa kurudi katika Mahakama ya mwanzo iliyotamka dhana ya ndoa ili kuweza kugawanya mali ambazo zilipatikana wakati mkata rufaa na mjibu rufaa wakiishi pamoja. Hukumu hii imeandikwa katika lugha ya Kiswahili ili kurahisisha kila upande kuelewa kilichoandikwa na kuweza kufanya maamuzi sahihi badala ya kutegemea kusomewa na watu baki ambao ni wachache wanaojua lugha ya kiingereza na kuitafsiri wanavyoona wao.

Imeamriwa hivyo.

Hakuna amri kuhusu gharama za shauri hili.

Haki ya rufaa ipo wazi.

Imeamriwa **MUSOMA** leo tarehe 05 mwezi Juni, 2023.

M. L. KOMBA

Jaji

Maamuzi yemesomwa leo tarehe 5/06/2023 mbele ya mrufani na mjibu rufani wakiwa katika chemba ya Jaji.

M. L. KOMBA

Jaji

05 Juni, 2023